TANGAZO LA SERIKALI NA. 256 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 10(1))*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA YA MKOPO KUTOKA SHIRIKA LA OVERSEAS PRIVATE INVESTMENT CORPORATION INAYOLIPWA NA KAMPUNI YA ALISTAIR JAMES YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio Kwenye Riba ya Mkopo kutoka Shirika la Overseas Private Investment Corporation inayolipwa na Kampuni ya Alistair James ya Mwaka 2024 na itaachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 6 Machi, 2024.

Msamaha

2. Kodi yote ya zuio kwenye riba ya mkopo kutoka kwa Shirika la Overseas Private Investment Corporation ya kiasi cha shilingi 515,385,746 inayolipwa na Kampuni ya Alistair James, imesamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafikia ukomo wake baada ya Kampuni ya Alistair James kuondolewa wajibu wa kulipa kodi ya zuio kiasi cha shilingi 515,385,746.

Dodoma,
5 April, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*